#MAKINIKIA Kutoka Kitabu Seeking Wisdom, Jinsi Ya Kufikiri Kwa Usahihi Na Kuepuka Kufanya Maamuzi Mabovu Kwenye Maisha.

Rafiki yangu mpendwa,

Karibu kwenye mafunzo ya ziada (#MAKINIKIA) kutoka kitabu chetu cha juma, ambapo kwa juma hili la 14 la mwaka 2019 tumejifunza kutoka kitabu kinachoitwa SEEKING WISDOM; From Darwin to Munger kilichoandikwa na Peter Bevelin

Kwenye #MAKINIKIA ya kitabu hiki, tunakwenda kujifunza **njia saba za uhakika za kuwa na maisha mabovu**, tutajifunza kupitia hekima za Warren Buffett na Charles Munger na pia utapata mwongozo wa kutumia wakati unafanya maamuzi ili kuepuka kufanya makosa.

Karibu kwenye #MAKINIKIA haya, ujifunze na kuwa bora ili uweze kufikiri kwa usahihi na kuepuka kufanya maamuzi mabovu kwenye maisha yako.

NJIA SABA ZA UHAKIKA ZA KUWA NA MAISHA MABOVU.

Katika hotuba yake kwa wahitimu wa chuo kikuu cha Havard mwaka 1986, Charles Munger aliwashirikisha njia saba za uhakika za kuwa na maisha mabovu.

Hapa Munger alitumia mfumo wake wa kufikiri kinyume, wa kufikiria ni wapi hutaki kwenda kisha kuepuka kwenda huko. Hivyo kwa kujua njia hizi za uhakika za kuwa na maisha mabovu, utaweza kuziepuka na kutokuwa na maisha mabovu.

Zifuatazo ni njia saba za uhakika za kuwa na maisha mabovu, unazopaswa kuziepuka sana kwenye maisha yako.

Moja; kutumia kemikali zinazoathiri akili.

Matumizi ya kemikali zinazoathiri akili kama pombe, madawa ya kulevya, sigara, bangi na vilevi vingine ni njia ya uhakika ya kuwa na maisha mabovu. Hakuna manufaa yoyote mtu anayapata kwa matumizi ya kemikali hizi. Kama unataka kuwa na maisha bora, epuka matumizi ya kemikali zinazoathiri akili.

Mbili; wivu.

Wivu ni njia ya uhakika ya kuwa na maisha mabovu, pale unapotumia muda wako mwingi kufuatilia maisha ya wengine na kujilinganisha nao, ni muda ambao unashindwa kuutumia kwa yale muhimu kwako.

Kama unataka kuwa na maisha bora, acha kufuatilia maisha ya wengine, ishi maisha yako na weka malengo yako na yafanyie kazi. Wengine wanafanya nini au wana nini hiyo siyo kazi yako, achana nayo.

Tatu; chuki.

Hakuna kitu kinaharibu maisha kama chuki, kwa sababu unapokuwa na chuki kwa mtu yeyote au kitu chochote, ni kujibebesha mzigo wewe wakati mwenzako yuko huru. Unajiweka kwenye kifungo ambacho anayekufunga hajui hata kama amekufunga.

Usiwe na chuki kwa yeyote au chochote, samehe kila mtu na muhimu zaidi jisamehe wewe mwenyewe. Kuwa huru wakati wote na nguvu zako peleka kwenye kufikia malengo yako na siyo kubeba chuki kwa wengine.

Nne; usiwe mtu wa kutegemewa.

Usiwe mwaminifu kwenye maisha yako, ahidi vitu na usitekeleze, ukipewa kazi usifanye kwa umakini na chelewesha kuikamilisha, kwa kifupi kuwa mzembe utakavyo. Hii ni njia ya uhakika ya wewe kushindwa na kuwa na maisha mabovu. Yaani ukifanyia njia hii moja kazi, utakuwa na maisha mabovu hata kama kitu gani kitafanywa kwako.

Ili kuwa na maisha bora unahitaji kujenga jina lako, kuwa mwaminifu na mtu unayeweza kutegemewa, ambaye neno lako linakuwa sheria na unatekeleza kila unachoahidi.

Tano; jifunze kwa uzoefu wako pekee.

Usikubali kabisa kujifunza kupitia uzoefu wa wengine, kila kitu mpaka ukijaribu wewe mwenyewe kwanza ndiyo ukubaliane nacho. Ukiona wengine wamekosea usijifunze kwao na kufanya tofauti, bali fanya kama walivyofanya wao na ukosee ili ujifunze kwa uzoefu wako. Hii ni njia ambayo siyo tu itafanya maisha yako kuwa mabovu, bali pia yatakuwa magumu sana.

Ili kuwa na maisha bora unapaswa kujifunza kupitia wengine, chukua uzoefu wa wengine na ufanyie kazi. Usirudie makosa ambayo wengine wameshafanya,

na kwa chochote unachotaka kufanya, angalia waliofanikiwa kwenye kitu hicho wanafanyaje kisha fanya kama wao.

Sita; ukianguka usiinuke tena.

Pale unapoweka mipango na ikashindwa, pale unapojaribu kitu na ukashindwa, usijisumbue kujaribu tena. Kubali kwamba umeshindwa na huwezi tena na baki hapo chini wala usiinuke tena. Hapo kwa hakika utakuwa na maisha ambayo ni mabovu sana na ya kushindwa kabisa.

Kila mtu anaanguka kwenye maisha, hivyo kuwa na maisha bora ni kuinuka pale unapoanguka, kujifunza na kuanza tena kwa ubora zaidi. Haijalishi umeanguka mara ngapi, unachopaswa kufanya ni kuinuka na kuendelea na safari yako.

Saba; usitake kujua sehemu mbaya na kuiepuka.

Wewe amua kwenda tu kama unavyotaka kwenda, usijisumbue kujua sehemu mbaya au hatari iko wapi na kuiepuka, badala yake nenda kama unavyojisikia mwenyewe. Kwa njia hii utashindwa na kuanguka kwenye kila unalojaribu.

Kuwa na maisha bora unapaswa kufikiri kinyume, na kufuata msingi wa Munger ambao ni kujua sehemu gani ukienda utakufa na hivyo kuepuka kwenda sehemu hiyo. Jua mambo gani ukifanya utakosa kile unachotaka na epuka kuyafanya. Siyo tu utakuwa na maisha bora, bali utaepuka hatari zisizo na maana kwenye maisha yako.

Rafiki, hizi ndizo njia saba za uhakika za kuwa na maisha mabovu, jukumu lako kwenye maisha ni moja, epuka njia hizi ili uwe na maisha bora.

HEKIMA KUTOKA KWA CHARLES T. MUNGER NA WARREN E. BUFFETT.

Munger na Buffett wamekuwa washirika katika uwekezaji kwa zaidi ya miaka 40 sasa. Kwa pamoja wameweza kufanikiwa sana kupitia uwekezaji. Pia wameweza kujijengea sifa kubwa katika uwekezaji, hasa katika kufanya maamuzi sahihi na yenye manufaa.

Hapa tunakwenda kujifunza hekima kutoka kwa watu hawa wawili katika maeneo mbalimbali ya maisha, biashara na uwekezaji.

1. **Kuhusu kubadili watu.**

Munger anatuambia kama tunataka kuwafanya watu wabadilike, basi tunapaswa kuwaonesha madhara ya baadaye ya kile wanachofanya sasa. Watu wanasukumwa kuchukua hatua pale wanapoona madhara makubwa ya baadaye.

2. **Kuhusu ugumu wa viongozi wa biashara kufanya maamuzi sahihi.**

Buffett anasema kuna sababu nne kwa nini ni vigumu viongozi wa biashara kufanya maamuzi sahihi kwa ukuaji wa biashara zao;

Moja; kufanya kwa mazoea, kuendelea kufanya kile ambacho kinafanyika sasa.

Mbili; kuruhusu miradi ya biashara kukua kulingana na kiasi cha fedha kilichopo.

Tatu; kile anachopendelea kiongozi wa biashara ndicho atakachoshauriwa na watu wa chini yake.

Nne; tabia ya kuiga kile ambacho kinafanywa na kampuni nyingine.

3. **Kuhusu ugumu wa kumwondoa mkurugenzi.**

Buffett anasema ni vigumu kumuondoa mkurugenzi mkuu (CEO) wa kampuni kwa sababu wenye jukumu hilo ni bodi ya wakurugenzi, ambayo haiathiriwi na chochote kwa maamuzi ya mkurugenzi mkuu. Kama angekuwepo mtu mmoja ambaye yuko juu ya mkurugenzi mkuu, angeweza kumwondoa kwa maamuzi yake, lakini kwa kuwa ni mchakato wa bodi nzima, na kwa kuwa mkurugenzi naye ni sehemu ya bodi, inakuwa vigumu kuondolewa, hata kama hafanyi vizuri.

4. **Kuhusu sifa za watu unaopaswa kufanya nao biashara.**

Buffett anasema unapochagua mtu wa kufanya naye biashara, iwe ni biashara yako au hata uwekezaji, angalia sifa hizi;

Moja; awe na hamasa kubwa sana kwenye kile anachofanya, akipende kutoka ndani yake.

Mbili; kujijua wao wenyewe na kujua ni maeneo gani wana uimara na maeneo gani wana udhaifu.

Tatu; kuwa tayari kuachana na fursa ambazo ziko nje ya uimara wake, hata kama zinaonekana kuwa na manufaa sana.

Nne; kuwa na tabia njema, uadilifu na uaminifu wa hali ya juu.

5. **Kuhusu kujijengea tabia bora.**

Buffett anasema ili kuweza kujijengea tabia bora, tafuta mtu unayemkubali sana na kisha kazana kuwa kama yeye, anaweza kuwa mtu aliye hai au ambaye ameshakufa. Muhimu ni uchague mtu ambaye ungependa kuwa kama yeye kisha jifunze na kujipima kupitia mtu huyo.

6. **Kuhusu kujiamini kupita kiasi.**

Buffett anasema wafanyabiashara wengi huwa wanaanguka kwa mafanikio kidogo wanayopata. Wanapofanikiwa kwenye jambo moja, wanajiamini kwamba wanaweza kufanikiwa kwenye kila kitu, na hapo ndipo wengi wanapojaribu vitu wasivyovijua na kushindwa.

Anashauri kila mtu ajue eneo lake la uimara na kuachana na maeneo mengine. Kufanikiwa kwenye eneo ulilo imara haimaanishi unaweza kufanikiwa kwenye kila kitu.

7. **Kuhusu faida ya ukuaji.**

Munger anasema kadiri biashara inavyokuwa kubwa, ndivyo inavyokuwa na nguvu kubwa ya ushindani. Biashara kubwa ina nguvu kubwa ya manunuzi na hivyo kuweza kununua kwa bei ya chini. Pia mauzo makubwa hata yakifanyika kwa faida kidogo, yanaleta faida kubwa kwa ujumla.

8. **Kuhusu hasara ya ukuaji.**

Munger pia anatuambia ukuaji una hasara zake, kadiri biashara inavyokuwa ndivyo urasimu unakua mkubwa na maamuzi yanachelewa kufanyika.

9. **Kuhusu kupata hekima ya dunia.**

Kama unataka kupata hekima ya dunia na uweze kufanya maamuzi bora kwenye mambo yako, Munger anasema unapaswa kujijengea msingi wa maamuzi, ambao unakuwa na nguzo kutoka maeneo mbalimbali ya kitaaluma kama fizikia, hesabu, falsafa, uchumi, baiolojia, saikolojia na nyinginezo. Huhitaji kuwa mbobezi kwenye maeneo yote, bali unapaswa kuelewa misingi ya kila eneo na kuitumia katika maamuzi.

10. **Kuhusu misingi mikuu mitatu ya uwekezaji.**

Buffett anasema kupitia Benjamin Graham amejifunza misingi mikuu mitatu ya uwekezaji;

Moja; unaponunua hisa, fikiria kama unaimiliki biashara nzima.

Mbili; unapaswa kuangalia kupanda na kushuka kwa soko na kuufanya kuwa rafiki kwako na kunufaika na kupanda na kushuka. Pake soko linaposhuka na kila mtu anauza unapaswa kununua na pale soko linapopanda na kila mtu ananunua unapaswa kuuza.

Tatu; jiwekee wigo mpana wa usalama, unapaswa kuwa na wigo mpana wa faida kwa bei unayonunulia na thamani halisi ya uwekezaji.

11.Kuhusu kuthaminisha biashara.

Buffett anasema njia pekee ya kuthaminisha biashara inatokana na msingi huu; ndege uliyenaye mkononi ana thamani ya ndege wawili waliopo msituni. Kwamba kile ulichonacho kina thamani kuliko kile ambacho bado hujawa nacho. Hivyo kabla hujawekeza fedha yako, lazima ujiridhishe kwamba utapata thamani kubwa kuliko kubaki na fedha hiyo.

12.Kuhusu kuepuka matatizo.

Buffett anasema kuwa na mikataba na sheria kali hazitakuepusha na matatizo. Njia pekee itakayokuepusha na matatizo ni kuepuka watu wenye matatizo. Chagua kufanya kazi na watu ambao unawaamini na wenye tabia nzuri na hutakutana na matatizo mengi. Lakini ukifanya kazi na watu wenye tabia zisizo nzuri, sheria na mikataba havitakusaidia.

Rafiki, hizi ndizo hekima kutoka kwa wawekezaji hao wawili ambazo tunaweza kuzitumia kwenye maeneo mbalimbali ya maisha yetu.

MWONGOZO WA KUFANYA MAAMUZI.

Unapokuwa kwenye kupanga malengo, kufanya uchaguzi, kutatua tatizo na hata kutathmini biashara au uwekezaji, tumia mwongozo huu;

1. Tumia msingi wa mawazo makubwa yanayohusu uhalisia wa kitu unachofanyia kazi.
2. Elewa kitu kina maana gani hasa.
3. Rahisisha, gawa kitu katika urahisi unaoweza kufanyia kazi.
4. Tumia kanuni zako binafsi na chujio katika kuamua kipi ufanyie kazi.
5. Jua ni nini hasa unachotaka kupata au kufikia.
6. Jua njia mbadala za kupata kile unachotaka.
7. Jua matokeo unayotarajia na usiyotarajia kwenye kile unachofanya.
8. Kuwa na hesabu kamili zinazokupa uhalisia wa jambo.
9. Tafuta ushahidi wa maamuzi unayofikia.

10. Fikiri kinyume kwa kuanzia kwenye kile ambacho hutaki kupata na kuepuka njia ya kukufikisha huko.
11. Kumbuka matokeo makubwa yanahusisha vipengele vingi.
12. Fanya tathmini ya madhara yatakayojitokeza iwapo utafanya makosa.

Fuata mwongozo huu kwenye maamuzi yote muhimu unayofanya na utapunguza sana kufanya makosa kwenye maamuzi yako.

Fanyia kazi haya uliyojifunza kwenye #MAKINIKIA haya ili uweze kufanya maamuzi bora kwenye maisha yako.

Uchambuzi huu wa kitabu umeandaliwa na Dr. Makirita Amani.

Dr Makirita ni daktari wa binadamu, kocha wa mafanikio, mwandishi na mjasiriamali. Kuendelea kupata chambuzi hizi za vitabu kwenye TANO ZA JUMA, hakikisha unajiunga na channel ya TANO ZA JUMA ambayo ipo kwenye mtandao wa telegram.

Kujiunga ni bure kwa juma la kwanza, kisha baada ya hapo unachagua kulipa tsh elfu moja kwa juma, au elfu tatu kwa mwezi au elfu 30 kwa mwaka. Kwa maelezo zaidi tuma ujumbe kwenda namba 0717396253, ujumbe utumwe kwa njia ya telegram pekee.

Karibu sana.